



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO

YA AMALI

MHE. SIMAI MOHAMMED SAID (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA
2021/2022**

Mei, 2021

YALIYOMO

UTANGULIZI	1
MIRADI YA SEKTA YA ELIMU	3
UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2019/20	3
MUUNDO WA PROGRAMU.....	3
MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU.....	4
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.....	5
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	7
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	10
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	10
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	12
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	13
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	14
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	16
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI	17
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali.....	17
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima	18
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU	20
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia.....	20
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	21
Huduma ya Ukaruzi wa Elimu.....	23
Huduma za Maktaba.....	24
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	25
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu	27
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	29
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	31
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	32
Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla.....	32
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	34
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Elimu Pemba	38

MAPATO	38
MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2019/20	
KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.....	38
Vipaumbele vya Wizara.....	39
MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU.....	41
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.....	42
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	43
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU	43
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu.....	44
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti.....	44
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	45
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	45
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	46
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI.....	46
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali.....	46
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.....	47
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU	47
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia.....	48
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	48
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu.....	48
Huduma za Maktaba.....	49
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	49
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	50
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu.....	50
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	51
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	51
Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla.....	51
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.....	52
Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba.....	52
MGAWANYO WA FEDHA KWA PROGRAMU.....	53
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI.....	53

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI	53
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU.....	53
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI.....	54
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU.....	54
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	54
MAKADIRIO YA MAPATO	55
JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI	55
SHUKURANI	55
KIAMBATISHO	58

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
2. **Mheshimiwa Spika**, Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema. Vile vile akatuwezesha kukamilisha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikuu ya Eid El Fitr na leo hii tukaweza kukutana katika kikao hiki cha bajeti katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Kiongozi wetu mahiri Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie kheri na baraka zake na aneweze she kuwasilisha hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ufasaha. Pia namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wasaa wajumbe wote wa kuichangia vizuri na hatimae Baraza lako tukufu liweze kuipitisha kwa kauli moja.
3. **Mheshimiwa Spika**, pili nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuanza vyema uongozi wake imara, wenye busara na moyo thabiti katika kusimamia uimarishaji wa huduma za jamii kwa wananchi wake ikiwemo huduma ya elimu. Mwenyezi Mungu amzidishie umri mrefu wenye kheri, afya njema na maarifa zaidi ili aendelee kutuongoza na kuiendeleza nchi

yetu vizuri. Vile vile, napenda kutoa pungezi zetu na shukurani za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji wao mzuri.

4. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, nachukua fursa hii kukupongeza wewe na Naibu Spika kwa kuliongoza Baraza hili vyema kwa mustakbal mwema wa maendeleo ya Taifa letu. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni busara, hekima, umahiri na uadilifu katika kutekeleza majukumu yenu.
5. **Mheshimiwa Spika,** Shukurani za dhati nizifikishe kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla kwa ushauri na maelekezo ya kimaendeleo wanayotupatia katika utekelezaji wa shughuli zetu mbalimbali wanapopata muda wa kuwa nasi katika taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, niwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwa umakini wao na michango yao wanayoitoa kwa maendeleo ya nchi yetu.
6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa, napenda kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Wakurugenzi, wakuu wa vitengo, Wajumbe wa Bodi mbali mbali za Elimu, Maafisa wa ngazi mbalimbali wa Wizara, bila kuzisahau Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu. Aidha, shukurani ziwafikie walimu, wazazi, wanafunzi na washirika wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia harakati za utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu iliyo bora kwa watoto, vijana na wazee wetu waliokosa fursa hiyo. Mola awazidishie moyo wa imani na upendo ili michango yao

iendelee kuwapatia elimu wahitaji wote kwa kiwango chenye ubora.

7. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka 2020/21. Nimatumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu katika Taifa letu.
8. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuelezea matarajio ya bajeti ya mwaka 2021/2022, nitawasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha wa 2020/2021.

MIRADI YA SEKTA YA ELIMU

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia miradi mikuu mitano kama ifuatayo: -
 1. Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi
 2. Uimarishaji wa Elimu ya Msingi
 3. Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
 4. Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali
 5. Miundombinu katika elimu

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2020/21

10. **Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa kupitia programu sita za elimu.

MUUNDO WA PROGRAMU

11. **Mheshimiwa Spika**, programu kuu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni sita kama ifuatazo: -

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawala

MAELEZO YA UTEKELEZAJI KWA PROGRAMU

12. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia Programu sita nilizoiainisha. Programu hizi zimezingatia malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020, vipaumbele vyatsekta, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).
13. **Mheshimiwa Spika**, Programu hizo zote zilitekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Jamii na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar. Programu hizi zilitengewa jumla ya TSh. 138,145,584,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 45,036,700,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, TSh. 73, 646,800,000/- malipo ya mishahara na TSh. 19,462,084,000/- kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, TSh. 4,500,000,000/- ni mchango wa SMZ na TSh. 14,962,084,000/- ni mchango wa Wahisani wakiwemo Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA), Mfuko wa OPEC (OFID), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Global Partnership for Education (GPE), UNICEF, UNESCO na Benki ya Dunia
14. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 94,199,954,937.14/- sawa na asilimia 68 ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, TSh. 64,320,817,919/- sawa na asilimia 84.17

zilitumika kulinia mishahara ya wafanyakazi na TSh. 13,695,619,963/= sawa na asilimia 29.5 zimetumika kwa ajili ya kazi za kawaida. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya TSh. 16,183,517,055.14/- zilipatikana. Kati ya fedha hizo, TSh. 2,981,000,000/- sawa na asilimia 66 ni mchango wa Serikali na TSh. 13,202,517,055.14/- sawa na asilimia 88 ni kutoka kwa wahisani.

15. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji halisi kwa Programu ni kama ifuatavyo: -

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

16. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inahusisha uimarishaji na utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne na kumi na mbili. Sehemu kubwa ya Programu hii imetekelezwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ kwa mashirikiano ya karibu na Wizara yangu kupitia mfumo wa Ugatuza.
17. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 5,135,232,000/-. Kati ya fedha hizo TSh. 1,086,169,000/- ni kwa ajili ya kazi za kawaida, Tsh. 393,500,000/- kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na TSh. 3,655,563,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya TSh. 4,175,257,255.14/= sawa na asilimia 82 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i). Jumla ya wanafunzi 14,751 wa Skuli 27 za Msingi Unguja na Pemba waliendelea kupatiwa huduma ya chakula kupitia Programu ya Lishe.
- ii). Jumla ya walimu 350 wa Maandalizi wa Skuli za Serikali na Walimu wasaidizi wa Vituo vya Tucheze Tujifunze (TuTu) wamepatiwa mafunzo ya miezi sita ya kuwajengea uwezo juu

ya mbinu bora za kufundishia na kujifunzia ili waweze kufundisha kwa ufanisi zaidi.

- iii). Jumla ya vituo 30 (18 Unguja na 12 Pemba) vipyta vya TuTu vimefunguliwa, na vituo 100 vimefanyiwa ukarabati (50 Unguja na 50 Pemba). Aidha, wasimamizi 60 na waratibu 14 wapya wa vituo vya TuTu wamepatiwa mafunzo ya mbinu za kufundishia.
- iv). Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo “manila sheet”, vibao vya kuandikia, penseli, vifutio na rangi vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo 30 vya TuTu Unguja na Pemba.
- v). Jumla ya Skuli 772 zinazota elimu ya Maandalizi zikiwemo 327 za Serikali, Vituo 364 vya TuTu na skuli 81 za jamii zilizosajiliwa Unguja na Pemba zimepatiwa fedha taslim TSh. 698,078,000/- ikiwa ni ruzuku za uendeshaji wa skuli.
- vi). Jumla ya walimu 300 wa Madrasa wamejengewa uwezo katika kukabiliana na udhalilishaji wa watoto pamoja na njia za kufundishia.
- vii). Ujenzi wa madarasa mapya 16 ya maandalizi (Unguja 12 na Pemba 04) umekamilika katika skuli za Kidichi Kikaangoni 02, Bambi 02, Kibumbwi 02, Mwera Gudini 02, Donge Chechele 02, Kiongoni Makunduchi 02 kwa Unguja na kwa Pemba ni Kipapo 02 na Kifundi 02.
- viii). Ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa 55 na Ofisi 11 (Unguja madarasa 26 na Ofisi 07 na Pemba madarasa 29 na Ofisi 04) ya Maandalizi na Msingi umekamilika. Aidha, madarasa 49 (Unguja 30 na Pemba 19) ya Maandalizi na Msingi yamefanyiwa ukarabati.
- ix). Mikutano na walimu, wazazi na maofisa elimu 323 wa Wilaya ya Kaskazini “A” na “B”, Wilaya ya Kusini, Wilaya ya Wete na

Chakechake imefanyika kujadili matatizo ya utoro, ndoa za utotoni, udhalilishaji na ajira za watoto. Aidha, wenyeviti 150 wa kamati za skuli na Masheha 150 wamejengewa uwezo juu ya ufuatiliaji wa majukumu yao katika kusaidia maendeleo ya kitaaluma na kupunguza vitendo vya udhalilishaji wa watoto Unguja na Pemba.

Matokeo ya Muda Mfupi;

- i. Jumla ya wanafunzi 91,074 sawa na asilimia 85.1 wameandikishwa katika madarasa ya maandalizi kwa mwaka 2021.
- ii. Jumla ya wanafunzi 59,525 wapya wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2021. Kati yao 29,721 ni wanaume na 29,804 ni wanawake. Kati ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza, wanafunzi 47,123 sawa na asilimia 79.2 wamepitia elimu ya maandalizi. Jadweli namba 15(c) linatoa ufanuzi zaidi.
- iii. Jumla ya wanafunzi 331,425 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi kwa mwaka 2021 ambao ni sawa na asilimia 122.5. Kati yao, wanaume ni 167,434 sawa na asilimia 123.1 na wanawake ni 163,991 sawa na asilimia 122.0. Jadweli namba 14 linatoa ufanuzi zaidi.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.

18. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya sekondari. Jumla ya TSh. 66,478,525,000/- zilipangwa kutumika, kati ya fedha hizo TSh. 8,052,940,000/- ni kwa ajili ya kazi za kawaida, TSh. 45,009,364,000/- kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na TSh. 13,416,221,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2021, jumla ya TSh.

42,552,690,091/- zilipatikana sawa na asilimia 78. Utekelezaji kwa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i). Vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Mitihani ya Taifa vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli za sekondari zenye madarasa ya Kidato cha nne na cha sita.
- ii). Skuli za Sekondari za Ufundi za Mikunguni Unguja na Kengeja kwa Pemba zimepatiwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia masomo ya ufundi katika fani za Umeme, Ujenzi, Makenika na Kompyuta.
- iii). Jumla ya walimu wapya 948 wakiwemo 224 wa Sayansi na 724 wa Sanaa wameajiriwa na kupangiwa kazi katika skuli za sekondari Unguja na Pemba.
- iv). Jumla ya TSh. 7,386,301,110/= za ruzuku zimetolewa kwa skuli 116 za Sekondari za Serikali kwa ajili ya uendeshaji.
- v). Ujenzi wa Skuli za Sekondari ya Donge, Hasnuu Makame iliyoko Kibuteni, Dk. John Pombe Magufuli iliyoko Mwanakwerekwe na Skuli ya Sekondari ya Dk. Shein iliyopo Wingwi Pemba umekamilika.
- vi). Ujenzi wa vituo 22 vya ubunifu wa Kisayansi vinavyojumuisha maabara, maktaba na madarasa 48 katika skuli za Regezamwendo, Uroa, Unguja Ukuu, Bwejuu, Mkwajuni, Tumbatu, Kijini, Mahonda, Kitope, Chuini, Mtoni Kigomeni, Kisauni, Jang'ombe kwa Unguja na Makangale, Mtambile, Kilindi, Pujini, Kisiwapanza Fundo Limbani, Kiuyu na Kojani kwa Pemba umekamilika na Vituo hivyo vimeshaanza kutumika.
- vii). Ujenzi wa Maabara katika Skuli 11 katika maeneo ya Chukwani, Fukuchani, Jongowe, Bumbwini, Machui na Jendele kwa Unguja na Shumba, Uondwe, Chanjamjawiri,

Chambani na Wambaa kwa Pemba unatarajiwa kuanza mwezi Juni mwaka huu.

- viii). Jumla ya skuli tano za Sekondari zimefanyiwa ukarabati mdogo. Skuli hizo ni Pale, Kusini, Kiembesamaki na Faraja kwa Unguja na Kengeja kwa Pemba. Aidha, ukarabati wa skuli ya Benbella unaendelea na umefikia asilimia 65.
- ix). Ujenzi wa miteremko (ramps) kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu unaendelea katika skuli 100 (60 Unguja na 40 Pemba) za Msingi na Sekondari.
- x). Ujenzi wa madarasa 50 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi umeanza katika skuli za Kidoti, Nungwi, Kilombero na Tunguu kwa Unguja na skuli za Mtambile, Makoongwe, Chambani, Mitiulaya, Wambaa, Gando, Furaha na Chwale kwa Pemba.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya wanafunzi 123,133 wameandikishwa katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ya awali (kidato 1 – 4). Kati yao, wanafunzi 69,680 wa kidato cha kwanza na pili wakiwemo wanaume 33,518 na wanawake 36,162. Kidato cha tatu na nne kina jumla ya wanafunzi 53,453 wakiwemo wanaume 22,270 na wanawake 31,183. Jadweli Nam. 19 linatoa ufanuzi zaidi.
- ii. Jumla ya wanafunzi 6,696 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya Sekondari ya juu (kidato 5-6) wakiwemo wanaume 3,203 na wanawake 3,493. Kati yao wanafunzi 4,043 ni wa Kidato cha tano wakiwemo wanaume 1,953 na wanawake 2,090 na wanafunzi 2,653 wa kidato cha

sita kati yao wanaume ni 1,250 na wanawake 1,403. Jadweli Nam. 21(a) na 21(b) zinatoa ufanuzi zaidi.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

19. **Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

20. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya TSh. 1,016,776,000/- za SMZ kwa kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada na kutoa mafunzo ya ualimu kazini. Kati ya fedha hizo TSh. 428,531,000/- zilitengwa kwa matumizi ya kawaida na TSh. 588,245,000/- kwa matumizi ya mshahara. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya TSh.366,476,030/- sawa na asilimia 62 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

- i. Jumla ya walimu 780 wanaofundisha masomo ya Biology, English na Geography Kidato cha I, II na IV wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu sahihi za ufundishaji na uchambuzi wa maswali ya mitihani.
- ii. Jumla ya walimu wa Sanaa 606 wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hisabati Kidato cha I&II wamekamilisha mafunzo yao ya kuwabdalisha kuwa walimu mahiri wa Sayansi na Hisabati. Aidha, jumla ya walimu 1,018 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na English wa skuli za Sekondari

wanaofundisha Kidato cha I na II wanapatiwa mafunzo ya mbinu za ufundishaji wa masomo hayo kwa lengo la kumudu kufundisha Mtaala Mahiri (Competence Base Curriculum).

- iii. Jumla ya walimu 1,186 wanaofundisha madarasa ya 5 na 6 masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza wamepatiwa mafunzo ya mbinu za ufundishaji kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wenyewe ufahamu mdogo.
- iv. Jumla ya wanafunzi 1,043 wameshiriki katika usaili wa kuijunga na mafunzo ya Ualimu katika ngazi ya Maandalizi, Msingi na Diploma katika Vyuo vya Kiislamu Unguja na Pemba kwa mwaka wa masomo 2021/2022. Kati ya hao wanafunzi 705 ni wa Cheti na 338 Diploma.
- v. Jumla ya walimu 538 waliopatiwa mafunzo ya Cheti cha Ualimu daraja la 3A kupitia Elimu Masafa, wamekamilisha programu hiyo na kukabidhiwa vyeti vyao.
- vi. Rasimu ya muongozo mpya wa Vituo vya Walimu imeandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa Elimu ili kupata maoni yao.
- vii. Zana za ufuatiliaji (dodoso) zimeandaliwa kwa lengo la kufanya tathmini ya matumizi ya mafunzo kwa walimu kuhusu mbinu za kufundisha kusoma, kuandika na kuhesabu kwa walimu wa madarasa ya 1, 2 na 3. Tathmini hii inashirikisha wanafunzi wanafunzi 7,125.

Matokeo ya muda mfupi

- i) Jumla ya wanafunzi 729 wanasomea mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Stashahada ya Ualimu. Kati yao, wanafunzi

517 wakiwemo wanaume 422 na wanawake 95 wanasomea Ualimu katika Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja na wanafunzi 212 wakiwemo wanaume 68 na wanawake 144 katika Chuo cha Kiislamu Kiuyu Pemba.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

21. **Mheshimiwa Spika**, Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar.

22. **Mheshimiwa Spika**, ngazi hii ya elimu ina jumla ya wanafunzi 7110 wanaosoma katika vyuo vikuu vitatu. Kati ya wanafunzi hao, 3,049 ni wanaume na 4,061 ni wanawake. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilitengewa ruzuku ya TSh. 14,778,600,000/-. Kati ya fedha hizo TSh. 1,261,500,000/- zilitengwa kwa matumizi ya kawaida na TSh. 13,517,100,000/- kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 10,723,906,734 /= sawa na asilimia 72 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -
 - i. Jumla ya wafanyakazi 25 wameajiriwa (12 ni wana taaluma na 13 ni waendeshaji).
 - ii. Wafanyakazi 66 wanalipiwa gharama za masomo ya muda mrefu katika kada za taaluma na uendeshaji. Kati ya wafanyakazi hao 44 wa ngazi ya Uzamivu, 14 ngazi ya Uzamili, 7 shahada ya kwanza na mmoja ngazi ya Stashahada.

- iii. Skuli mpya ya Kompyuta, Mawasilino na Taaluma ya Habari imezinduliwa.
- iv. Programu mpya za Shahada ya kwanza ya Ujasiriamali na Shahada ya Uzamili ya Teknologia ya Habari zimeanzishwa.

Matokeo ya muda Mfupi

- i) Jumla ya wanafunzi 2,046 wamedahiliwa katika ngazi mbali mbali.
- ii) Jumla ya wanafunzi 1,525 (wanaume 665 na wanawake 860) wamehitimu katika ngazi za Shahada na Stashahada katika programu mbali mbali na kutunikiwa yeti.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

23. **Mheshimiwa Spika**, huduma ya Sayansi na Teknolojia ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya Sayansi na Teknolojia nchini. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi ilitengewa ruzuku ya TSh. 1,897,100,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 441,300,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 1,455,800,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh.1,245,722,935/= sawa na asilimia 65.7 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii kwa mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo: -

- i). Ujenzi wa jengo la utawala ambalo limeondoa tatizo la ofisi za watumishi wa Taasisi umekamilika.
- ii). Jumla ya wanafunzi wapya 835, wanaume 765 na wanawake 70 kwa fani zote za Taasisi wamesajiliwa.

iii). Mafunzo mapya ya shahada ya kwanza ya uhandisi umeme, uhandisi majenzi na kuiendeleza Taasisi kwa kuisaidia jamii kutumia Sayansi na Teknolojia yameanzishwa.

Matokeo ya muda Mfupi

i). Jumla ya wanafunzi 1,567 wakiwemo wanaume 1,014 na wanawake 553 wanaendelea na masomo katika fani mbalimbali zikiwemo Shahada ya Urubani na Uhandisi wa ndege, Stashahada za Uhandisi, Stashahada ya Teknolojia ya Habari Mawasiliano na Biashara, Stashahada ya Mafunzo ya Hisabati na Sayansi kwa Skuli za Msingi, Stashahada ya Usimamizi wa Maabara na Cheti kwa Mafunzo ya Amali (VETA). Jadweli namba 29(a) na 29(b) zinatoa ufanuzi zaidi.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

24. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar inatoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Bodi ilitengewa jumla ya TSh. 11,566,400,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 11,250,000,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 316,400,000/- ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 4,716,352,156/= sawa na asilimia 40.8 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

i) Jumla ya wanafunzi 4,261 wamepatiwa mikopo ya elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wapya 1,535 na 2,726 wanaoendelea na masomo. Idadi hii ni sawa na ongezeko la wanafunzi 180 ya wanafunzi 4,081 waliohudumiwa mwaka 2019/20.

- ii) Wanafunzi 24 wamepatiwa nafasi za ufadhilli wa masomo nje ya nchi zilizotolewa na washirika wa maendeleo mbalimbali wakiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (20) na Falme ya Kiarabu, Ras Al-Khaimah (4).
- iii) Wanafunzi 205 wakiwemo wapya 100 na wanaoendelea na masomo 105 wamepatiwa ufadhilli wa masomo wa SMZ kutokana na ufaulu wao wa ngazi ya juu katika mtihani wa Kidato cha Sita.
- iv) Jumla ya wanafunzi wapya 48 wamepatiwa ufadhilli wa masomo kwa vyuo vya ndani ya nchi wakiwemo 37 kuitia taasisi za Darul Imaan katika Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu na 11 kuitia Shirika la “Direct Aid” lililotoa ufadhilli wa masomo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait cha Chukwani.
- v) Jumla ya wanafunzi 1,036 wakiwemo wanafunzi 661 wanaosoma vyuo vya Zanzibar, 223 katika vyuo vya Tanzania Bara na 152 wa vyuo vya nje ya Tanzania wanatarajiwa kuhitimu masomo yao katika fani na ngazi mbalimbali za elimu.

Matokeo ya muda Mfupi

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya TSh. 2,240,000,000/= zimerejeshwa sawa na asilimia 69.78 ikiwa ni marejesho ya mkopo ya TSh. 3,210,000,000/= ya lengo lililowekwa.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

25. **Mheshimiwa Spika**, huduma ya uratibu wa Elimu ya Juu ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu. Huduma hii inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Kitengo kilitengewa jumla ya TSh.

50,000,000/= kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya Tsh. 10,500,000/= sawa na asilimia 21 zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i) Nafasi za masomo kwa ufadhili kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za China, Morocco, Malaysia, France, Mauritius, Hungary, Misri katika Chuo Kikuu cha El-Just, Misri katika Chuo cha Al Azhar Saudi Arabia na Jumuiya ya Madola zimetangazwa. Nafasi hizo zilijumuisha fani mbalimbali zikiwemo Udaktari, Uchumi, Uhandisi, Ualimu, Uuguzi na Sayansi ya Mazingira, Kilimo, Siasa na uhusiano wa Kimataifa, Maendeleo ya Jamii, Sayansi ya Kompyuta, Usimamizi wa Biashara na Utawala kwa viwango vya Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu.
- ii) Jumla ya waombaji 306 wakiwemo wanaume 197 na wanawake 109 wamewasilisha maombi yao.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya wahitimu 208 (wanaume 48 na wanawake 160) wa fani mbalimbali zikiwemo Kilimo, Mazingira, Uongozi wa Fedha, Udaktari wa Meno kwa kiwango cha Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili waliripoti. Orodha ya wahitimu hao na fani zao za masomo zimewasilishwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- ii. Jumla ya wanafunzi 50 kati ya 306 wamenufaika na nafasi za masomo kwa Nchi ya Morocco, Misri China na Hungary.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

26. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea vijana uwezo wa kupambana na soko la ajira kwa kuwapatia

mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

27. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya TSh. 8,423,410,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 6,536,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 1,887,410,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 2,351,760,007/= kutoka SMZ zilipatikana sawa na asilimia 28. Utekelezaji halisi kwa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya vikundi 16 (10 Unguja na 06 Pemba) vimepatiwa mkopo wenye thamani ya TSh. 9,135,550/-. Vikundi hivyo vimejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo juu ya utafutaji wa masoko na udhibiti wa fedha.
- ii) Mamlaka imeratibu ufanyaji wa Mtihani wa Taifa wa MMA kwa wanafunzi wa vituo 13 vikiwemo vitatu vya MMA na 10 vya binafsi ambapo jumla ya wanafunzi 1,680 (1,125 wanaume na wanawake 555) walishiriki katika mitihani hiyo. Wanafunzi 1,264 (wanaume 799 na wanawake 465) sawa na asilimia 75 wamefaulu mitihani yao
- iii) Jumla ya vituo 15 vimefanyiwa ukaguzi wa usajili ambapo vituo 8 vimepatiwa usajili wa muda vikiwemo Fantastic Training Centre, Upendo Sewing centre, Juwalaza Training Centre, Microtech Training Centre, ACESS Center for Enterpreneuership na Daya Vocational Training centre.
- iv) Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya Umekamilika na ujenzi wa Chuo kama hicho Makunduchi umefikia asilimia 98.

Aidha, vifaa mbalimbali vimesambazwa katika vyuo hivyo vikiwemo; vifaa vya uvuvi, vitanda, magodoro n.k.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya vijana wapya 1,298 wamejiunga na vituo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali mwanzoni mwa mwaka 2021.
- ii. Jumla ya TSh. 217,280,045/= zimerejeshwa na vikundi vya vijana vilivyopatiwa mkopo wa kuweza kujajiri.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

28. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu mionganini mwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 980,864,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 535,904,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 444,960,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 421,847,190/- sawa na asilimia 43 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Madarasa 24 mapya ya kisomo kwa Unguja na Pemba yamefunguliwa na kufanya idadi ya madarasa yote ya kisomo kufikia 510. Aidha, jumla ya wanakisomo 6,894 wa kisomo cha Watu Wazima wamefanyiwa upimaji katika hatua zote nne za kisomo. Wanafunzi 513 wa hatua ya nne wamekombolewa kuititia upimaji huo.
- ii) Jumla ya vikundi 127 (83 Unguja na 44 Pemba) vyenye jumla ya wanachama 2,454 (Wanaume 165, Wanawake 2,293)

vimeendelezwa kwa lengo la kuwapunguzia utegemezi wanawake wenyе umasikini wa kipato.

iii) Jumla ya wanafunzi 103 (wanaume 55 na wanawake 48) wamesajiliwa katika vituo vya kujiendeleza Unguja na Pemba. Aidha, wanafunzi 73 (wanaume 5 na wanawake 68) walioshindwa kuendelea na masomo yao baada ya mtihani wa Kidato cha Pili na cha Nne wameandikishwa katika Kituo cha Sayansi Kimu Forodhani kusomea fani ya Upishi, Ushoni, Kudarizi na Kufuma.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya wanakisomo 8,084 wameandikishwa wakiwemo wanaume 983 na wanawake 7,101.
- ii. Jumla ya wanafunzi 769 wenyе umri wa miaka 9 hadi 14 waliokuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu wameandikishwa katika madarasa ya Elimu Mbadala. Kati ya hao, wanafunzi 337 wameandikishwa Unguja na 432 kwa Pemba wakiwemo wanaume 424 na wanawake 345.
- iii. Jumla ya wanafunzi 379 wenyе umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo Unguja na Kituo cha Wingwi Mtemani Pemba. Kati yao, wanaume ni 255 na wanawake 124. Vijana hawa wanasomea fani za Umeme, Ushoni, Upishi, Udobi, Uchoraji, Kilimo, Ufugaji, Useremala, Mafunzo ya Kompyuta na Utunzaji Nyumba pamoja na masomo ya kawaida.
- iv. Jumla ya watahiniwa 4,112 wamefanya mtihani wa faragha wa Kidato cha Nne, kati yao wanafunzi 2,482 sawa na asilimia 60 ya watahiniwa wote wamefaulu. Aidha,

wanafunzi 109 kati ya 209 (wanaume 143 na wanawake 66) waliofanya mtihani wa faragha wa Kidato cha Sita mwezi Mei, 2020 kwa Unguja na Pemba ambao ni sawa na asilimia 52 wamefaulu.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

29. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Progamu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo: -

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

30. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya TSh. 675,000,000/, kati ya fedha hizo, TSh. 331,800,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 343,200,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya TSh. 373,328,185/= sawa na asilimia 55 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- Rasimu ya mihutasari ya masomo ya maandalizi imeandikwa ikiwa ni muendelezo wa utayarishaji wa mtaala mpya wa elimu ya maandalizi na msingi. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanda mtaala wa stashahada ya ualimu ngazi ya elimu ya maandalizi na msingi umefanyika.
- Rasimu ya muongozo wa vigezo vya kuandika vitabu imetayarishwa kwa madhumuni ya kudhibiti ubora wa vitabu

vya kujifunzia na kufundishia mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi.

- iii. Pendekezo na zana za utafiti kuhusu ufundishaji wa masomo ya sayansi ngazi ya elimu ya sekondari (Kidato cha I-II) limetayarishwa. Jumla ya mikutano miwili na wadau wa elimu imefanyika Unguja na Pemba kuhusu kujadili mihutasari ya somo la Historia ya Tanzania ngazi ya elimu ya Maandalizi hadi sekondari ikiwa ni utekelezaji wa agizo la aliyekua Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli.
- iv. Miundo ya Utumishi ya Taasisi imekamilika na imewasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa hatua.
- v. Kanuni za Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar zimetayarishwa na zimewasilishwa katika Bodi ya Ushauri ya Taasisi.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

31. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya TSh. 5,116,900,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 4,659,000,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 457,900,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 3,740,231,081/- sawa na asilimia 73 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma ya Upimaji na Tathmini ni kama ifuatavyo: -
- i) Jumla ya wanafunzi 50,952 (wanaume 26,080 na wanawake 24,872) wa Darasa la Nne waliandikishwa kufanya mtihani wa Darasa la Nne. Wanafunzi halisi waliofanya mtihani ni 48,248 (wanaume 24,127 na wanawake 24,119) sawa na asilimia 94.7 ya walioandikishwa.

- ii) Jumla ya wanafunzi 34,218 (wanaume 16,383 na wanawake 17,835) waliandikishwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi Darasa la Sita. Kati yao wanafunzi 33,010 (wanaume 15,528 na wanawake 17,482) sawa na asilimia 96.46 walifanya mtihani.
- iii) Jumla ya wanafunzi 33,792 (wanaume 15,445 na wanawake 18,347) waliandikishwa kufanya mtihani wa kumaliza Kidato cha Pili, ambapo wanafunzi 32,279 (Wanaume 14,543 na Wanawake 17,736) sawa na asilimia 95.52 walifanya mtihani.
- iv) Jumla ya wanafunzi 225 (wanaume 18 na wanawake 207) waliandikishwa kufanya mtihani ya Cheti cha Ualimu Maandalizi (ECD), ambapo wanafunzi wote 225 sawa na asilimia 100 wamefanya mtihani.
- v) Baraza la Mitihani limewaandikisha Walimu wanafunzi 202 wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kumaliza masomo ya Stashahada ya Ualimu kwa ngazi ya Msingi na Sekondari katika Vyuo vya Kiislamu vya Unguja na Pemba, kati yao 38 ni wanaume na 164 ni wanawake. Mitihani hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 03 – 11 Mwezi huu wa Mei, 2021.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i) Jumla ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa Darasa la Nne ni 39,273 sawa na asilimia 81.40, kati ya hao, wanaume ni 18,111 sawa na asilimia 37.54 na wanawake ni 21,162 sawa asilimia 43.86 ya watahiniwa wote.
- ii) Wanafunzi waliofaulu mtihani wakumaliza Darasa la sita ni 32,462 sawa na asilimia 98.34, wanaume ni 17,376 sawa

na asilimia 52.64 na wanawake ni 15,086 sawa na asilimia 45.70 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, wanafunzi 1,363 wamefaulu kuendelea na masomo yao katika madarasa ya vipawa (174) na michepwo (1,189) sawa na asilimia 4.1.

- iii) Wanafunzi 25,393 sawa na asilimia 78.7 wamefaulu mtihani wa Kidato cha Pili na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu wakiwemo wanaume 15,107 sawa na asilimia 46.8 na wanawake 10,286 sawa asilimia 31.87
- iv) Wanafunzi wote 225 sawa na asilimia 100 wamefaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (ECD) ambapo wanaume ni 18 na wanawake ni 207.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

32. **Mheshimiwa Spika**, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inafuata sera, sheria, miongozo na taratibu zilizopo. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya TSh. 1,103,700,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 366,900,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 736,800,000/- ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya TSh. 771,873,158/- zilipatikana sawa na asilimia 70. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya skuli 719 (630 za Serikali na 89 za binafsi) Unguja na Pemba sawa na asilimia 80 ya makadirio ya skuli zilizopangwa kukaguliwa zimekaguliwa. Kati ya skuli hizo 39 ni za Maandalizi, 349 ni za msingi na 331 za sekondari.
- ii) Jumla ya walimu 2,509 wamekaguliwa na kupewa ushauri kulingana na masomo wanayofundisha, Unguja na Pemba.

Huduma za Maktaba

33. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na watu wote. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku yenye jumla ya TSh. 1,133,400,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 693,900,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 439,500,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2021, Jumla ya TSh. 503,195,651/= sawa na asilimia 44 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya vitabu vya msaada 20,708 kutoka Shirika la ‘Book Aid International’ la Uingereza vimepokelewa na kusambazwa katika taasisi mbali mbali za elimu Unguja na Pemba.
- ii) Jumla ya vitabu 15,792 vimegaiwa katika taasisi 60 za elimu (32 Unguja na 28 Pemba). Taasisi husika ni skuli 5 za maandalizi zimepatiwa vitabu 390, skuli 18 za msingi zimepatiwa vitabu 4,493, skuli 34 za sekondari zimepatiwa vitabu 9,222, Vyuo 2 vilipatiwa vitabu 893 na taasisi isiyo ya kiserikali (Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Organization) ilipatiwa vitabu 794.
- iii) Jumla ya watumiaji 25,100 walifika maktaba kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali ikiwemo uazimaji na usomaji vitabu na kutafuta taarifa za kitaaluma.
- iv) Vitabu 14,556 vya aina mbalimbali viliazimwa na kutumiwa ndani na nje ya maktaba.
- v) Jumla ya programu 69 za watoto zimefanyika na kuwashirikisha watoto 3,238. Miiongoni mwa programu

hizo, programu 67 zilifanyika ndani ya maktaba na programu 2 zilifanyika nje ya maktaba.

- vi) Jumla ya programu 8 za Kiingereza za "Youth English Corner" zimefanyika na kuwashirikisha vijana 31 (wanaume 258 na wanawake 133).

Matokeo ya Muda Mfupi

- i). Jumla ya wanachama wapya 450 (378 watu wazima na 72 watoto) walisajiliwa katika Maktaba za Bodii
- ii). Idadi ya watumiaji wa maktaba imefikia 25,100. Miiongoni mwao 8,422 ni wanawake, wanaume ni 9,404 na 7,274 ni watoto.

Huduma ya Urajisi wa Elimu

34. **Mheshimiwa Spika**, huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha sheria, sera na taratibu za Wizara zinafuatwa katika skuli za Serikali na za binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za binafsi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, huduma hii ilipangiwa kutumia jumla ya ruzuku ya TSh. 264,400,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 110,200,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 154,200,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 154,260,879/- sawa na asilimia 58 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Zoezi la ufuutiliaji la wanafunzi waliopata ujauzito kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 unaendelea ambapo jumla ya wanafunzi 126 (Wilaya ya Kati 31, Wilaya ya Kusini 23, Wilaya ya Mkoani 28 na Wilaya ya Chake chake 44) waligundulika kuwa na ujauzito.

- ii) Jumla ya kesi 7 za udhalilishaji Unguja na Pemba zimeripotiwa katika Ofisi za Mrajisi zikiwemo ubakaji na ulawiti. Kati ya kesi hizo moja ni ya mwanafunzi wa Sekondari na sita za wanafunzi wa Msingi.
- iii) Jumla ya kesi 23 za ujauzito zimeripotiwa katika Ofisi ya Mrajisi wa elimu Uguja na Pemba pia kwa Kamanda wa Polisi wa Mikoa husika. Kati ya kesi hizo, kesi 19 zimejadiliwa kwa mujibu wa Sheria namba 4 (2005) ya kuwalinda Wari na Mtoto wa Mzazi Mmoja ambayo imewapa fursa wanafunzi hawa kuendelea na masomo yao.
- iv) Jumla ya kesi 2 za ndoa (1 Uguja na 1 Pemba) zimeripotiwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 6 ya mwaka 1982 kifungu cha 20(3) wanafunzi hao hawaruhusiwi kuendelea na masomo yao.
- v) Zoezi la utoaji wa leseni mpya za walimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki linaendelea ambapo limeanza kwa walimu wa Sekondari wa Mkoa wa Mjini Magharibi Uguja na taarifa zao zimeshaingizwa katika kompyuta na kupigwa picha.

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Jumla ya walimu 2,908 wakiwemo wa Cheti cha Ualimu, Stashahada, Shahada ya Kwanza na ya Pili walipatiwa leseni za kufundishia za muda wa miaka mitano.
- ii) Jumla ya skuli 32 za Serikali zimepatiwa usajili zikiwemo skuli 2 ya maandalizi pekee, 11 za maandalizi na msingi, 5 za msingi na 14 za sekondari kwa Uguja na Pemba.
- iii) Jumla ya skuli 42 za binafsi zimewasilisha maombi ya usajili wa muda na zimepewa usajili wao baada ya kukaguliwa.

Kati ya hizo, 28 za maandalizi, 10 za maandalizi na msingi, skuli moja ya maandalizi msingi na sekondari na skuli 3 za sekondari. Aidha, jumla ya skuli tano za Unguja na Pemba zimewasilisha maombi ya usajili wa kudumu, kati ya hizo skuli 2 za maandalizi na msingi, na skuli 3 za sekondari.

- iv) Jumla ya vyuvo vinne vimewasilisha maombi ya usajili wa fani ya ualimu vikiwemo chuo cha Dunga development collage, chuo cha Early Childhood Training Collage, chuo cha Samail Gombani Chake chake Pemba na Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia.
- v) Jumla ya skuli 927 za ngazi mbalimbali za serikali na binafsi zimehakikiwa. Kwa upande wa Unguja jumla ya skuli 775 zimehakikiwa katika Mkoa wa Kusini na Mkao wa Mjini Magharibi, pia jumla ya skuli 152 zimehakikiwa katika Mkao wa Kaskazini Pemba.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

35. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa katika maisha ya kila siku. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, programu hii ilipangiza kutumia jumla ya TSh.548,133,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 278,059,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 270,074,000/- ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 281,945,897/- zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 58.9. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i). Wizara inaendelea na matayarisho wa mpango mkakati wa TEHAMA katika Elimu ili kuimarisha utekelezaji wa Sera ya TEHAMA katika Elimu.
- ii). Matayarisho ya mfumo wa “Free Air Time Cost” kwa ajili ya kurusha vipindi vinavyotayarishwa na Kituo cha Habari katika elimu (KMEC) pamoja na kituo cha Televisheni cha SUZA umekamilika. Mfumo huu umeanza kutumika kwa wadau mbali mbali wa Elimu kupitia anuwani <http://zlms.kmec.go.tz>
- iii). Watendaji 15 wa Kituo cha Habari katika Elimu (KMEC) wamepatiwa mafunzo ya kutengeneza programu za TV kwa kutumia lugha ya alama ili kusaidia watu wenye mahitaji maalumu.
- iv). Taasisi 143 zimeshakaguliwa na kufanyiwa upembuzi yakinifu zikisubiri upatikanaji wa fedha ili nazo ziweze kuunganishwa na mkonga wa Taifa. Aidha, vituo 22 vya Ubunifu wa Sayansi (Hubs) Unguja na Pemba vimewekewa miundombinu ya TEHAMA katika maabara za masomo ya sayansi, vyumba vya kompyuta na lugha.
- v). Wizara imesambaza jumla ya Redio 50 za aina ya MP3 kwa Vituo vya TUTU ambazo zinatumika kuendeshea vipindi vya masomo ya maandalizi.

Matokeo ya muda mfupi;

- i. Jumla ya vipindi 400 vimetayarishwa, kati ya hivyo 160 vya Redio na Vipindi 240 vya TV na kuendelea kurushwa kupitia Redio na Televisheni (ZBC, ZCTV, Redio zakitaifa na Redio Jamii, “e-Learning platform”-ZLMS na youtube ya Wizara).

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

36. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2020/21 programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 597,610,000/- kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya TSh. 16,020,000/- sawa na asilimia 3 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

- i). Vyumba viwili vya kufanya upimaji wa kitaalamu wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu “resource rooms” katika skuli ya Michakaini Pemba na skuli ya Kisiwandui Unguja vimeanza kutumika na wanafunzi wenye matatizo ya usikivu.
- ii). Jumla ya wafanyakazi 517 wa kada mbali mbali wakiwemo walimu, wakaguzi wa skuli na watendaji wa Baraza la Mitihani la Zanzibar walipewa mafunzo ya elimu mjumuisho yaliyolenga kuwajengea uwezo watendaji hao.
- iii). Jumla ya walimu 800 walipatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho ambayo yalilenga zaidi katika somo la hisabati kwa walimu wote wa madarasa ya I na II kwa skuli zote za Msingi. Aidha, walimu 20 kutoka skuli zenyenye wanafunzi wenye ulemavu wa uoni walipatiwa mafunzo ya namna bora ya kutumia “Orbit reader” ambayo inasaidia kusoma na kuandika maandishi ya nukta nundu. Skuli hizo zilikabidhiwa “orbit readers” 11 (skuli ya Kisiwandui 3, Michakaini 3, Kizimkazi 1, Chokocho 1, Mkwajuni 1, Shumba 1 na Idara ya Mafunzo ya Amali walipatiwa 1).

- iv). Jumla ya walimu 20 wanaotumia lugha ya alama na Braille walipatiwa mafunzo ya kutumia programu ya EPUB katika mchakato wa kujifunza.
- v). Jumla ya skuli 227 (Unguja 120 na Pemba 107) zilifanyiwa ufuatiliaji na upimaji kwa ajili ya ujenzi wa 'ramps' ili kujua uhitaji wa 'ramps' kwa ajili ya kuyafanya mazingira yawe rafiki na yanayofikika kwa wanafunzi wote. Skuli 121 zimechaguliwa kujengewa 'ramps na aprons'

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Jumla ya wanafunzi 667 wenye mahitaji maalum wamefanyiwa upimaji ili kugundua uhitaji wa vifaa saidizi katika kujifunza. Upimaji ulifanyika katika maeneo ya usikivu, uoni, viungo na afya ya akili. Kati ya wanafunzi hao waliofanyiwa upimaji, wanafunzi 279 walitibiwa na 194 walipewa rufaa kwa uchunguzi zaidi.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kuitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 762,061,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 579,611,000/- ni kwa kazi za kawaida na TSh. 182,450,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 214,076,710/- sawa na asilimia 31.8 zilipatikana. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya walimu 21 na wanafunzi 119 wameshiriki katika mafunzo yanayolenga kuhamasisha uzalendo, nidhamu na kuwajenga wanafunzi katika maadili mema pamoja na kuwafahamisha historia ya nchi yao. Mafunzo haya yamefanyika katika Mikoa minne kwa Unguja na Pemba. Aidha, walimu 104 (38 Wilaya ya Magharibi A, 32 Wilaya ya Magharibi B na 34 Wilaya ya Micheweni) walipatiwa mafunzo ya kutayarishwa kuwa viongozi wa Skauti.
- ii) Jumla ya wanafunzi 352, walimu 44 na waratibu 11 walishiriki katika mashindano ya mbio za nyika. Mashindano hayo yalizishirikisha Wilaya zote 11 Unguja na Pemba.
- iii) Shughuli za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa "Sports 55" zimefanyika katika kila Wilaya na kwa kila skuli husika. Ufuatiliaji huu wa kina umelenga kuhakikisha kwamba vifaa vilivyotolewa vinatunzwa na kutumika vizuri na walimu waliopatiwa mafunzo wanawajibika ipasavyo.
- iv) Kituo cha Olimpia Afrika kilichopo Dole kilipatiwa vifaa vikiwemo mipira 4, machela 1, soksi darzeni 3, viatu pea 7, sheenguard pea 7 na nishani 35.
- v) Jumla ya viongozi wanne na wanafunzi 22 (11 wanaume na 11 wanawake) wameshiriki katika mashindano ya Tanzania "Baseball" Championship yaliyofanyika Dar es Salaam. Timu ya Baseball kwa wanaume na timu ya "softball" kwa wanawake zilishiriki.
- vi) Jumla ya wanafunzi 54 (36 kutoka Skuli za Msingi na 18 kutoka Skuli za Sekondari) walishiriki mashindano ya Maigizo na Uchoraji ngazi ya Taifa katika Tamasha la Utamaduni wa

Mzanzibari yaliyoratibiwa na Wizara ya Vijana, Utamaduni,
Sanaa na Michezo.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

38. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha na kusimamia upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa ujumla, programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za elimu Pemba.

Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla

39. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kutoa ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, programu hii ilipangiwa jumla ya TSh. 6,446,873,000. Kati ya fedha hizo, TSh. 3,319,832,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 3,127,041,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh. 4,251,764,145/= zilipatikana sawa na asilimia 71. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya walimu 1,069 (605 Unguja na 464 Pemba) na 282 nje ya kada ya ualimu walijiriwa baada ya kupata kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini. Kati yao, kwa upande wa Unguja walimu 2 Shahada ya Pili Sayansi, 97 ni wa Shahada ya Kwanza Sayansi, 448 Shahada ya Kwanza Sanaa, 37 Stashahada ya Sayansi na 21 Stashahada ya Sanaa, na kada mbali mbali 186 kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba Shahada ya Kwanza Sayansi ni 41 Shahada ya

Kwanza Sanaa ni 257, Stashahada ya Sayansi ni 58, Stashahada ya Sanaa ni 12 na kada mbali mbali ni 96.

- ii) Jumla ya wafanyakazi 48 Unguja na 30 Pemba waliopewa likizo walilipwa posho la likizo la jumla ya TSh. 7,800,000/-.
- iii) Jumla ya walimu 38 walistaafu kwa mujibu wa sheria, 35 kwa Unguja na 3 kwa Pemba. Wafanyakazi 3 waliacha kazi kwa sababu mbalimbali. Aidha wafanyakazi 7 walipewa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika Wizara na taasisi mbalimbali, wafanyakazi 2 wamechukua likizo bila ya malipo, walimu 7 walifariki dunia (Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amin).
- iv) Jumla ya wafanyakazi 624 (385 Unguja na 239 Pemba) wamedhaminiwa kupata mikopo ya Benki na Saccos mbalimbali nchini. Wafanyakazi hao wamepata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Mikopo iliyotolewa ina thamani ya TSh.1,834,286,378/- kwa Unguja na TSh 49,672,427/- kwa Pemba.

Matokeo ya muda mfupi;

Hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 9,135 (4,849 ni wanawake na 4,286 wanaume). Wafanyakazi 6,683 wapo Unguja (3,794 wanawake na 2,889 wanaume) na kwa upande wa Pemba jumla ya wafanyakazi 2,452 (wanawake 1,055 na wanaume ni 1,397). Kati ya wafanyakazi wote hawa 6,266 ni wa kada ya ualimu na 2,869 ni wafanyakazi wasiokuwa wa kada ya ualimu.

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

40. **Mheshimiwa Spika**, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 6,187,899,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 5,628,399,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 559,500,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021 Jumla ya TSh. 2,845,765,625/- sawa na asilimia 47 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i. Rasimu ya mapitio ya Sera mpya ya Elimu imewasilishwa katika makongamano mawili makubwa yaliyowajumuisha washiriki 200 kwa ajili ya kutoa michango yao ya kuiimarisha. Washiriki katika mijadala hiyo ilijumuisha walimu, wanafunzi, wazee, maafisa kutoka taasisi za Serikali na binafsi, watu mashuhuri, washirika wa maendeleo pamoja na viongozi mbalimbali wa Wilaya na Mikoa yote ya Unguja na Pemba. Rasimu hiyo itawasilishwa kwenye vikao vya juu vya Serikali kwa ushauri zaidi.
- ii. Ufutiliaji wa utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Elimu umeendelea kwa kila robo mwaka na ripoti za utekelezaji zimetayarishwa. Aidha, Wizara imeendelea kufutilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya elimu iliyokamilika na inayoendelea. Mionganoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari (ZISP), Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na utekelezaji wa Mradi wa Elimu Mbadala na Amali (ALSD II).

- iii. Mkutano mkuu wa nne wa mwaka wa tathmini ya elimu (4th AJESR) uliowashirikisha wadau 150 wa elimu wa ndani na nje ya Zanzibar wakiwemo wahisani, wazee, wanafunzi, kamati za skuli, taasisi za Serikali na za watu binafsi umefanyika. Kauli mbiu ya mkutano huo wa nne ilikuwa ni “Kuongeza kasi ya Matumizi ya Teknolojia katika kujifunza na Kufundishia”. Jumla ya maazimio matano yalipitishwa yenyelengo la kuinua ubora wa elimu kuitia matumizi ya TEHAMA katika kujifunza na kufundishia.
- iv. Jumla ya vikalio 35,600 (Seti za viti na meza) kwa ajili ya wanafunzi wa Sekondari vimenunuliwa kutoka China. Hatua ya usafirishaji wa vikalio hivyo kutoka China inaendelea ambapo awamu ya kwanza ya seti 9,600 za viti na meza imeshafika. Matayarisho ya kuvisambaza katika skuli yanaendelea.
- v. Rasimu ya Andiko la Mradi wa kuimarisha elimu ya Sekondari kwa wanawake chini ya ufadhili wa KOICA imetayarishwa na kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa hatua za kuwasilishwa kwa Mfadhili.
- vi. Wizara ipo katika hatua ya mwisho ya mchakato wa kutafuta mshauri elekezi wa kusanifu na kusimamia ujenzi wa Skuli tatu za ghorofa katika maeneo ya Gamba, Mfenesini kwa Unguja na Kifundi kwa Pemba.
- vii. Mafunzo ya kuzisaidia skuli za Sekondari za Serikali ya kuweza kuandaa mipango kazi ya maendeleo ya skuli zao yamefanyika kwa skuli zote za Wilaya ya Kusini Unguja, Kati na Kaskazini “A” na “B” kwa Unguja na Wilaya za Wete,

- Micheweni, Mkoani na Chakechake kwa Pemba. Mafunzo haya yanaendelea kwa Skuli zilizobakia.
- viii. Wizara inaufanyia tathmini Mpango Mkuu wa Elimu (ZEDP II) ikiwa ni matayarisho ya maandalizi ya kundaa Mpango Mkuu wa miaka mitano mengine, 2021 - 2026.
 - ix. Matayarisho ya utafiti wa kutathmini maendeleo ya wanafunzi wa msingi (Darasa la 1 – IV) wenyе lengo la kujua uwezo wa Watoto katika Kuandika, Kusoma na Kuhesabu yanaendelea, ambapo kazi ya andiko la dhana ya utafiti (Research Proposal) na matayarisho ya zana za kukusanya taarifa imekamilika.
 - x. Matayarisho ya Kitabu cha Takwimu za Elimu (Annual Statistical Abstract 2020) yanaendelea katika hatua za uchambuzi wa taarifa.
 - xi. Zoezi la Sensa ya Mwaka ya Skuli (Annual School Census) limekamilika.
 - xii. Maandalizi ya Mradi mpya wa uimarishaji wa elimu ya lazima chini ya ufadhilli wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Sida yapo katika hatua za mwisho ambapo rasimu ya “document” ya mradi (Project Appraisal Document) imekamilika. Mradi huu wenyе lengo la kuimarisha ubora wa elimu ya msingi utakuwa ni wa miaka mitano (2021 - 2026) na utagharimu jumla ya US\$ 6 milioni sawa na TZS 13.8 bilioni. Aidha, Wizara inakamilisha miradi mingine mitatu; mradi wa kuimarisha elimu ya amali kupitia ufadhilli wa Benki ya ADB (Mkopo), Mradi wa kuimarisha elimu ya lazima (WB Mkopo) na mradi wa utanuzi wa Chuo cha SUZA (BADEA Mkopo). Rasimu ya

maandiko ya miradi hii yote imekamilika na wahisani hao wote wameonesha nia ya kusaidia.

- xiii. Hatua za awali za matayarisho ya mradi wa kuimarisha matumizi ya maktaba kwa kutumia teknolojia “offline library” yameanza kwa mashirikiano na taasisi ya Global Outreach Programme yenye ofisi yake mkoani Iringa. Wakurugenzi na maafisa wa Wizara wametembelea mfumo huo Iringa kwa lengo la kuusoma na kujua changamoto zake ikiwa ni matayarisho ya kuutumia mfumo huo kwa skuli za hapa Zanzibar.

Matokeo ya muda mfupi;

- i) Jumla ya Skuli 166 za Sekondari Unguja na Pemba zimepatiwa mafunzo ya kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Skuli zao.
- ii) Jumla ya maandiko manne ya miradi mipya ya uimarishaji wa elimu yameandaliwa.
- iii) Mashirikiano ya wahisani wa maendeleo katika sekta ya elimu yameimarika kwa kuongeza washirika wakiwemo Serikali ya Austria, Taasisi ya “Educate a Child” (EAC) ya Qatar na Global Outreach Tanzania.

Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba

41. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya TSh. 3,431,811,000/. Kati ya fedha hizo, TSh. 771,245,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TSh. 2,660,566,000/- ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya TSh.

2,799,615,809/= zilipatikana sawa na asilimia 86. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

MAPATO

42. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukusanya mapato kuitia usajili wa Skuli za binafsi na malipo ya leseni za walimu. Hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya TSh. 118,157,940/= kati ya TSh. 215,700,000/= zilizopangwa kukusanya. Hii ni sawa ya asilimia 54.8 ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanya TSh. 34,739,580/= zinatokana na malipo ya leseni za walimu na TSh. 83,418,360/= ni za usajili wa skuli za binafsi.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2021/2022 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU

43. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kuanzia na vipaumbele vya Wizara.

Vipaumbele vya Wizara

44. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imelenga kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya Elimu kwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -
- i. Kuzipatia skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari ruzuku za uendeshaji wa skuli pamoja na kuwapatia wanafunzi vifaa mbalimbali vikiwemo vikalio, mabuku ya

kuandikia na vifaa vyengine vya kusomeshea na kujifunzia vikiwemo chaki, vitabu vya kiada na ziada na vifaa vya maabara.

- ii. Kuimarisha miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga madarasa 485 yakiwemo madarasa 300 yaliyoanzishwa na wananchi na Madarasa 185 mapya; skuli tano za Maandalizi (moja katika kila mkoa); Skuli tatu za Msingi katika maeneo ya Kidichi, Nanguji na Pujini; Skuli 9 za Sekondari katika maeneo ya Mtopepo, Mfenesini, Gamba, Bumbwini, Chukwani, Donge, Kifundi, Mfikiwa na Muambe; na Skuli mbili maalum za mjumuisho katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Pemba.
- iii. Kujenga skuli moja ya Ufundu Nungwi katika Wilaya ya Kaskazini “A”.
- iv. Kujenga maabara katika skuli 11 za Sekondari za Fukuchani, Jongowe, Chukwani, Bumbwini, Machui, Jendele, Shumba, Uondwe, Chanjamjawiri, Chambani na Wambaa.
- v. Kufanya ukarabati mkubwa wa skuli za Sekondari za Paje-Mtule, Uzini, Haile salassie, Chwaka Tumbe, Dkt. Omar Ali Juma na Chuo cha Kiislamu Kiuyu.
- vi. Kuimarisha huduma za maktaba kwa kujenga maktaba kuu ya kisasa katika Wilaya ya Kaskazini “A”.
- vii. Kujenga Chuo cha Mafunzo ya Amali katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali vya Wilaya katika Wilaya za Kaskazini “B”, Magharibi “A”, Kati, Mkoani na Micheweni.
- viii. Kujenga jengo la Ofisi la Wizara

- ix. Kujenga dahalia mbili katika skuli za Chwaka Tumbe na Paje-mtule.
- x. Kutekeleza programu ya lishe kwa skuli zote za Maandalizi za Serikali na skuli 36 za msingi.
- xi. Kukamilisha mihutasari ya elimu ya Maandalizi na Msingi na kununua vitabu.
- xii. Kuimarisha mazingira rafiki ya skuli kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum.
- xiii. Kuzipatia zawadi skuli 300 zitakazofanya vizuri katika mitihani ya Taifa ya darasa la sita, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne.
- xiv. Kuimarisha matumizi ya ICT katika kujifunza na kufundishia.
- xv. Kuvipatia Vituo vya Amali vifaa vya kisasa.
- xvi. Kuwapatia walimu mafunzo.
- xvii. Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.
- xviii. Kuimarisha huduma za ukaguzi.
- xix. Kuandaa Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo ya Elimu.

45. **Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo: -

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa

huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu.

47. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itatekeleza miradi sita ya maendeleo ambayo ni:-
- i). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi
 - ii). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Msingi
 - iii). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
 - iv). Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu katika elimu
 - v). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Amali
 - vi). Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU

48. **Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

49. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, utekelezaji wa programu ya Maandalizi na Msingi ulikuwa ukisimamiwa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kupitia mfumo wa Ugatuzi. Usimamizi na utekelezaji wa programu hii sasa umerejeshwa rasmi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzia bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.

50. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya sekondari.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kumtayarisha mtoto kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Viashiria vyat matokeo;

- Asilimia ya uandikishaji.
- Uwiano wa idadi ya walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi.

Shabaha za utekelezaji;

- Kuongeza kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 84.4 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 87 ifikapo mwaka 2022.
- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi wa msingi kutoka asilimia 83.9 kwa mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 89 ifikapo mwaka 2022.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

51. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kutoa Elimu ya Sekondari.

Viashiria vyat matokeo;

- Asilimia ya uandikishaji
- Asilimia ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima,
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi na wanaoendelea katika ngazi ya kidato cha nne, cha sita na elimu ya juu.
- Uwiano wa idadi ya wanafunzi na walimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

Shabaha za utekelezaji;

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia 77.1 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2022.
- Kiwango cha ufaulu cha mpito kutoka kidato cha pili kwenda cha tatu kuongezeka kutoka asilimia 78.7 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2021.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

52. **Mheshimiwa Spika**, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

53. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Elimu ya Diploma ya Ualimu kutolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wote walioandikishwa vyuo vya ualimu.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka 99 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2022.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

54. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu kutolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Stashahada.
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Shahada ya kwanza ya Uzamili na Uzamivu.
- Idadi ya tafiti zinazofanywa.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kutoka 7,110 mwaka 2021 hadi kufikia 8000 mwaka 2022.

Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia

55. **Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuimarisha ufundishaji na kujifunza Sayansi, Hisabati na Teknolojia
- Elimu ya Ufundi kuimarishwa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wahitimu katika Taasisi,
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

56. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutolewa.
- Fedha zilizokopeshwa kwa wanafunzi kurejeshwa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo
- Idadi ya wanafunzi wanaorudisha mikopo.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza utoaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka wanafunzi 3,607 ya waombaji mwaka 2020/21 hadi kufikia wanafunzi 4,000 ifikapo mwaka 2021/22.
- Kuongeza makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka TSh. 2,240,000,000/= ya mwaka 2020/21 na kufikia TSh. 3,500,000,000/= mwaka 2021/22.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

57. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Tathmini katika vyuo vinavyotoa elimu ya juu kufanyika.
- Wahitimu waliomaliza masomo ya elimu ya juu kuratibiwa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kijinsia.
- Idadi ya wahitimu wa elimu ya juu kijinsia.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

58. Mheshimiwa Spika, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo mbili kama ifuatavyo;

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

59. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujajiri ili kujikwamua na umasikini.

Matokeo ya muda mfupi;

- Mafunzo ya Amali na ufundi kutolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Ukosefu wa ajira kwa vijana kupungua
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza mafunzo ya amali kuongezeka.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

60. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu mionganoni mwa wanajamii.

Matokeo ya muda mfupi;

- Elimu mbadala na ya watu wazima kutolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Kiwango cha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa watu wazima,
- Idadi ya watu wazima wanaoshiriki katika madarasa ya wanakisomo,
- Idadi ya vijana waliojiunga na madarasa na vituo vya elimu mbadala,

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika kutoka asilimia 84.2 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2022.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

61. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu na programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo;

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

62. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote kutayarishwa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya Mitaala na vifaa vya kufundishia na kujifunzia viliviyotayarishwa na kusambazwa katika skuli.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

63. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi;

- Malengo ya elimu kupimwa.

Viashiria vya matokeo;

- Asilimia ya wanafunzi na kiwango cha mpito katika ngazi za darasa la nne, darasa la sita, kidato cha pili, kidato cha nne na cha sita.
- Asilimia ya ufaulu wa walimu na wanafunzi

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

64. **Mheshimiwa Spika,** utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya skuli zilizokaguliwa
- Idadi ya ripoti za ukaguzi zilizowasilishwa

Huduma za Maktaba

65. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kutoa nafasi kwa wanafunzi na watu wengine ya kupata taarifa mbalimbali kuititia maktaba.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya watu wanaotumia maktaba
- Idadi ya vitabu, CDs, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba.
- Idadi ya skuli zenyenye maktaba kamili.

Huduma ya Urajisi wa Elimu

66. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafaatuwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

Matokeo ya muda mfupi;

- Skuli za Serikali na binafsi zenyenye viwango bora kusajiliwa
- Leseni za walimu kutolewa.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya leseni za walimu zilizotolewa.
- Idadi ya skuli zilizosajiliwa.
- Sheria ya Elimu iliyopitiwa na kurekebishwa.
- Idadi ya kesi za ndoa kwa wanafunzi zilizofuatiliwa na kutolewa uamuzi.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

67. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

Matokeo ya muda mfupi;

- Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa watoto wenye mahitaji maalum kutolewa

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wanafunzi na walimu katika Elimu Mjumuisho.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

68. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kujifunza, kufundisha, ngazi ya utawala na katika maisha ya kila siku.

Matokeo ya muda mfupi;

- Walimu na wanafunzi wanapatiwa mafunzo juu ya matumizi ya Teknolojia ya kisasa.

Viashiria vya utekelezaji;

- Idadi ya walimu wenye ujuzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano,
- Idadi ya Skuli zenyе vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano
- Idadi ya Taasisi za elimu zilizounganishwa na mkonga wa Taifa.
- Mafunzo ya matumizi ya kompyuta kutolewa kuanzia katika skuli za msingi.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli

69. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kuinua taaluma ya michezo katika skuli.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya walimu wenyewe taaluma ya michezo
- Idadi ya skuli zenyewe viwanja vya michezo
- Idadi ya skuli zenyewe vifaa vya michezo
- Idadi ya wanafunzi wenyewe vipaji vya michezo

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

70. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii madhumuni yake makubwa ni kuhakikisha nyenzo zilizo bora zinapatikana na zinatumika kwa kuimarisha utoaji wa elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu kama zifuatavyo: -

Programu ndogo ya Uongozi kiujumla

71. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuratibu usimamizi na ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kupatikana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma, uongozi na utawala wa rasilimali za Wizara.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa na kustaafu,
- Mafunzo yanayotolewa kwa wafanyakazi.

Shabaha za Utekelezaji;

- Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wafanyakazi na upatikanaji wa nyenzo za kufanya kazi.

Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti

72. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kufanikisha na kuratibu Mipango, Sera na Utafiti katika Wizara.

Matokeo ya muda mfupi;

- Kupatikana kwa sera na mipango ya Wizara, kufanya utafiti na kufanya ufuatiliaji na tathmini.
- Kuibua Miradi ya Maendeleo ya Elimu.

Viashiria vya matokeo;

- Idadi za tafiti zilizofanywa
- Uwepo wa Sera mpya ya mwaka 2021
- Uwepo wa Ripoti za utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya Elimu.
- Idadi ya miradi mipyä iliyoibuliwa

Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba

73. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Matokeo ya muda mfupi na viashiria vya utekelezaji vinavyotumika ni kama vile vilivyoolezwa katika programu za uongozi kiujumla na uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.

MGAWANYO WA FEDHA KWA PROGRAMU

74. **Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inaonesha mgawanyo wa fedha kwa Programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

Idara Husika: Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi

Gharama za Programu: Jumla ya TSh.79,037,993,000/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 57,312,685,000/- ni kwa kazi za kawaida na TSh.21,725,308,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

Idara Husika: Idara ya Elimu ya Sekondari

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 110,014,054,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya hizo TSh. 58,840,132,000/- kwa kazi za kawaida na TSh. 51,173,922,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

Taasisi Husika: Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Kitengo cha Uratibu wa Elimu wa Juu.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh.31,587,437,000/- zimepangwa kwa kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

Idara Husika: Mamlaka ya Mafunzo ya Amali pamoja na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 16,348,230,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya fedha hizo TSh. 10,127,563,000/-ni kwa matumizi ya kawaida na TSh. 6,220,667,000/- kwa kazi za maendeleo.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

Idara Husika: Taasisi ya Elimu ya Zanzibar, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar, Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Katika Elimu, Ofisi ya Mrajisi wa Elimu, Idara ya Michezo na Utamaduni Katika Skuli.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 10,191,397,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii kwa kazi za kawaida.

PROGRAMU YA SITA: UONGOZI NA UTAWALA

Idara Husika: Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi ya Elimu Pemba.

Gharama za Programu: Jumla ya TSh. 18,370,632,000/= zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii. Kati ya hizo, TSh. 14,219,086,000/- ni kwa kazi za kawaida na TSh. 4,151,546,000/- kwa kazi za maendeleo.

MAKADIRIO YA MAPATO

75. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inakadiria kukusanya jumla ya TSh. 283,170,000/- ikiwa ni mapato kutoka katika vyanzo vyake vikuu ambavyo ni leseni za walimu na ada ya usajili wa skuli za binafsi.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

76. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya TSh. 265,549,743,000/= zitahitajika katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya sekta ya Elimu. Kati ya hizo TSh. 227,861,688,000 /= ni za SMZ na TSh. 37,688,055,000/= ni kutoka kwa Wahisani. Fedha zinazotoka SMZ, TSh.45,583,388,000/= ni za miradi ya Maendeleo, TSh.131,184,500,000/= ni kwa ajili ya Mishahara na TSh 51,093,800,,000/= ni kwa matumizi ya kawaida. Aidha, fedha kutoka kwa wahisani TSh. 14,568,055,000/= ni za ruzuku kwa miradi ya maendeleo kutoka GPE, UNICEF, KOICA, Table for Two (TfT), Shirika la Good Neighbour la Korea na Milele Zanzibar Foundation na TZS. 23,120,000,000/= ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA).

SHUKURANI

77. **Mheshimiwa Spika**, nachukuwa fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa washirika wote wa maendeleo ya elimu wa ndani na nje walioituunga mkono na kutoa mashirikiano katika utekelezaji wa mpango wa sekta ya elimu. Mionganini mwa washirika hao ni wanafunzi wenyewe, wazazi, washirika wa maendeleo na mashirika ya misaada ya kimataifa. Tunatoa shukurani zetu za pekee kwa mashirika mbalimbali yakiwemo, Sida, USAID, UNESCO, UNICEF, VSO, OPEC Fund, GPE, Good Neighbours na *Table for Two*. Pia shukurani zetu za dhati kwa Aga Khan Foundation, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Napenda pia, kuyashukuru mashirika yasiyo ya kiserikali

yakiwemo Milele Zanzibar Foundation, Jumuiya ya Madrasa Early Childhood Education Program, NFU, FAWE, Save the Children Fund, Book Aid International, Kinderhart foundation na ZAPDD. Vile Vile napenda kuyashukuru makampuni na mashirika mbalimbali ya kifedha yakiwemo Benki ya watu wa Zanzibar, CRDB, NBC, NMB, Postal Bank Tanzania, ZANTEL na SACCOS mbalimbali kwa misaada yao katika sekta yetu ya elimu na kwa wafanyakazi kwa ujumla. Shukurani za pekee ziende katika Halmashauri zetu za Wilaya kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuchangia maendeleo ya elimu Zanzibar.

78. **Mheshimiwa Spika**, Shukurani za pekee kwa Chama changu cha Mapinduzi kuanzia Taifa hadi Shina kwa kuwajali wananchi wote na kuwaletea maendeleo. Niushukuru uongozi mzima wa Mkoa wa Kusini Unguja na wananchi wenzangu wote hasa kina mama kwa kuendelea kuniamini na kushirikiana nami katika kuendelea kusimamia maendeleo kwa taifa letu.
79. **Mheshimiwa Spika**, shukurani kwa familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia.
80. **Mheshimiwa Spika**, mwisho, napenda kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu kuanzia wewe Mheshimiwa Spika kiongozi wetu na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa mnaoendelea kunipa na kwa namna mtakavyoichangia hotuba yangu hii, nasema ahsanteni sana.
81. **Mheshimiwa Spika**, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya jumla ya TSh. 265,549,743,000/= kwa mwaka wa fedha 2021/22, ili kuiwezesha Wizara yetu hii kutekeleza majukumu yake.

82. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO

(Takwimu za Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Kwa Kipindi cha 2016/17 - 2020/21 na Hali Halisi ya Elimu na
Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2020/21)

JADWELI NAM. 1

UKUAJI WA IDADI NA AINA ZA VITUO VYA ELIMU VILIVYOSAJILIWA, 2017 - 2021

AINA ZA VITUO	2017	2018	2019	2020	2021		
					SERIKALI	BINAFSI	JUMLA
VITUO VYA TUTU	297	302	342	366	390	0	390
SKULI ZA MAANDALIZI	328	347	382	363	40	452	492
SKULI ZA MSINGI (DAR I - VII)	299	357	381	431	304	173	477
SKULI ZA MSINGI/KATI 'A' (DAR I - KID 2)	41	38	29	17	2	10	12
SKULI ZA MSINGI/KATI 'B' (DAR I - KID 4)	67	54	59	46	0	59	59
SKULI ZA MSINGI/SEKOND.(DAR I - KID 6)	5	9	9	9	0	8	8
SKULI ZA KATI 'A' FORM 1 - FORM 2	3	3	7	26	24	0	24
SKULI ZA SEKOND. FORM 1 - FORM 4	117	135	136	169	162	7	169
SKULI ZA SEKOND. YA JUU (FORM 1 - 6)	13	11	26	26	24	5	29
SKULI ZA SEKOND. YA JUU (FORM 5 - 6)	-	-	-	2	1	0	1
SKULI ZA MCHEPUO WA KIFARANSI	1	1	1	0	1	0	1
SKULI ZA MCHEPUO WA UFUNDI	2	2	2	0	2	0	2
SKULI ZA MCHEPUO WA BIASHARA	1	1	2	0	3	0	3
SKULI ZA MCHEPUO WA KIISLAMU	1	2	2	0	2	0	2
SKULI ZA MCHEPUO WA SAYANSI JAMII	2	1	2	0	0	0	0
SKULI ZA MCHEPUO WA SAYANSI	10	7	8	0	10	0	10
SKULI ZA MCHEPUO WA KOMPYUTA	1	1	3	0	2	0	2
SKULI ZA MCHEPUO WA KILIMO	-	-	-	-	1	0	1
VITUO VYA MAFUNZO YA AMALI	3	2	2	3	4	5	9
VYUO VYA UALIMU	2	2	2	2	2	0	2
TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA	1	1	1	1	1	0	1
CHUO KIKUU CHA TAIFA Z'BAR (SUZA)	1	1	1	1	1	0	1
CHUO KIKUU CHA SUMAIT - CHUKWANI	1	1	1	1	0	1	1
CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR	1	1	1	1	0	1	1
JUMLA	1197	1279	1399	1464	976	721	1697

JADWELI NAM. 2(a)**UKUAJI WA IDADI YA WATOTO WA UMRI WA KWENDA SKULI KWA MWAKA, 2017 - 2021**

UMRI WA NGAZI YA ELIMU	2017	2018	2019	2020	2021	ONGEZEKO KWA MWAKA %
4 - 5 (Ulezzi)	94,848	103,950	105,653	107,082	91,074	-0.8
6 - 11 (Msingi)	239,284	237,634	246,069	259,469	331,425	5.6
6 - 15 (Msingi - Kidato 4)	-	-	-	416,071	454,558	8.5
12 - 15 (Kidato 1 - Kidato 4)	-	-	-	124,496	123,133	-1.1
12 - 17 (Kidato 1 - Kidato 6)	-	-	-	130,173	129,829	-0.3

* Kuanzia mwaka 2016 umri wa watoto wa kwenda skuli katika ngazi tafauti za elimu umefuata sera mpya ya elimu ya mwaka 2006 ilivyoagiza

JADWELI NAM. 2(b)

UKUAJI WA UANDIKISHAJI WA WANAFUNZI KATIKA NGAZI MBALI MBALI, 2017 - 2021

NGAZI YA ELIMU	2017	2018	2019	2020	2021			ONGEZeko KWA MWAKA %
					SERIKALI	BINAFSI	JUMLA	
Maandalizi	62,720	72,151	85,974	92,098	39,671	32,000	71,671	3.39
Msingi (Darasa I - VI)	256,048	276,858	290,510	313,097	291,218	40,348	331,566	6.67
Kati 'A' (Kidato 1 - 2 Bila ya Mchepuo)	81,246	67,657	69,547	67,520	59,912	6,230	66,142	-5.01
Kati 'B' (Kidato 3 - 4 Bila ya Mchepuo)	31,828	49,024	56,004	51,705	45,106	6,037	51,143	12.59
Sekondari ya Juu (Kidato 5 - 6)	3,643	4,590	4,808	5,679	5,925	729	6,654	16.25
Vipawa ya Juu (Kidato 1 - 4)	563	585	559	479	573	-	573	0.44
Mchepuo wa Sayansi (Kidato 1 - 4)	1,580	2,033	2,305	2,169	2,607	-	2,607	13.34
Mchepuo wa Ufundı (Kidato 1 - 4)	362	378	403	445	456	-	456	5.94
Mchepuo wa Kifaransa (Kidato 1 - 4)	189	197	211	215	221	-	221	3.99
Mchepuo wa Kiislamu (Kidato 1 - 4)	409	414	455	446	399	-	399	-0.62
Mchepuo wa Biashara (Kidato 1 - 4)	585	568	572	541	597	-	597	0.51
Mchepuo wa Kompyuta (Kidato 1 - 4)	452	447	382	380	506	-	506	2.86
Mchepuo wa Sayansi Jamii (Kidato 1 - 4)	591	435	273	593	-	82	82	-38.97
Mchepuo wa Wanawake (Kidato 1 - 4)	715	-	-	-	-	-	-	N/A
Kilimo	-	-	-	-	39	-	39	0.00
Ufundı Sanifu	545	522	649	1,529	-	-	-	-100.00
Ualimu (Kiislamu) Diploma - Kiuyu + Mazizir	395	841	1,224	1,221	1,206	-	1,206	32.19
Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar - SUZA	2,952	4,465	3,892	4,808	4,887	-	4,887	13.43
Chuo Kikuu Cha SUMAIT - Chukwani	1,506	969	841	875	925	-	925	-11.47
Chuo Kikuu Cha Zanzibar	2,579	3,094	2,334	1,620	-	1,808	1,808	-8.50
Jumla	448,908	485,228	520,943	545,420	454,248	87,234	541,482	4.80

JADWELI NAM. 2(c)

ASILIMIA YA UANDIKISHAJI (GROSS LEVEL ENROLMENT RATIO)

KATIKA NGAZI MBALI MBALI ZA ELIMU, 2017 - 2021

UMRI WA NGAZI YA ELIMU	2017	2018	2019	2020	2021
Maandalizi	66.1	69.4	81.4	86.0	85.1
Msingi	106.9	116.5	118.1	120.7	122.5
Msingi - Kidato 4*	95.3	90.2	96.0	105.2	105.6
Kidato 1 - Kidato 4*	-	-	-	79.5	77.1
Kidato 1 - Kidato 6*	-	-	-	58.3	55.7

*Pamoja na Michepwo

JADWELI NAM. 3

UKUAJI WA IDADI YA WANAFUNZI KATIKA MADARASA, 2017 - 2021

MADARASA	2017		2018		2019		2020		2021				ONGEZeko	
	WAS	J'LA	WAS	J'LA	KWA MWAKA (%)									
Darasa I	25218	51389	29167	60040	29619	60892	30360	62517	26286	54091	4826	9536	31112	63627
Darasa II	23931	48708	24304	49341	27163	55141	27807	57392	24642	50805	4072	8184	28714	58989
Darasa III	20945	42157	24065	48364	23950	48961	27251	55028	23844	48974	3628	7168	27472	56142
Darasa IV	19869	40055	21370	43267	25754	52000	24778	50566	23935	48690	2983	5919	26918	54609
Darasa V	19629	39030	19513	38736	20614	40795	26391	52673	22159	44680	2614	5076	24773	49756
Darasa VI	18165	34709	19199	37110	17074	32721	18127	34921	22790	43908	2212	4394	25002	48302
Kid. I (Michepuo)	593	948	812	1345	784	1244	902	1537	878	1343	20	20	898	1363
Kid I (Wengine)	17624	34711	17595	33702	18758	35981	17482	33841	15787	30732	1645	3253	17432	33985
Kid.2 (Michepuo)	964	1566	628	1035	806	1328	802	1263	801	1350	20	20	821	1370
Kid. 2 (Wengine)	25462	46535	17637	33955	17909	33566	17780	33679	15276	29575	1507	3008	16783	32583
Kid. 3 (Michepuo)	803	1568	1146	1825	699	1135	866	1428	791	1270	23	23	814	1293
Kid. 3 (Wengine)	9577	16652	19574	33275	15997	28467	15996	28007	14231	24421	1814	3217	16045	27638
Kid. 4 (Michepuo)	693	1364	745	1437	914	1453	628	1040	726	1213	19	19	745	1232
Kid. 4 (Wengine)	8903	15176	9167	15749	16887	27537	13955	23698	11942	20352	1583	2865	13525	23217
Kid 5	1267	2370	1437	2951	1453	3019	1784	3341	1766	3559	324	484	2090	4043
Kid 6	821	1666	1044	2063	1114	2258	1585	3069	1224	2366	179	287	1403	2653
Jumla	194464	378604	207403	404195	219495	426498	219561	426654	207078	407329	27469	53473	234547	460802
													4.80	5.03

JADWELI NAM. 4

UKUAJI WA IDADI YA WALIMU KATIKA NGAZI YA MSINGI NA SEKONDARI (DARASA LA 1 - KIDATO 6) 2017 - 2021 SKULI ZA SERIKALI NA BINAFSI

MWAKA	SKULI ZA SERIKALI				SKULI ZA BINAFSI				JUMLA			
	WALIOSOMEA	WASIOSOMEA	JUMLA	% WASIOSOMEA	WALIOSOMEA	WASIOSOMEA	JUMLA	%WASIOSOMEA	WALIOSOMEA	WASIOSOMEA	JUMLA	%WASIOSOMEA
2017	10187	87	10274	0.8	1865	401	2266	17.7	12052	488	12540	3.9
2018	10674	59	10733	0.5	2108	319	2427	13.1	12782	378	13160	2.9
2019	11420	52	11472	0.5	2584	374	2958	12.6	14004	426	14430	3.0
2020	12099	29	12128	0.2	3206	336	3542	9.5	15305	365	15670	2.3
2021	12791	37	12828	0.3	2898	423	3321	12.7	15689	460	16149	2.8

Takwimu hizi hazijumuishi Walimu wa Chuo cha Karume na Skuli za Maandalizi

JADWELI NAM. 5**UKUAJI WA WANAFUNZI NA WALIMU (PUPIL TEACHER RATIO) KATIKA NGAZI YA MSINGI NA KATI
(DAR. 1 - KID. 6) 2017 - 2021 SKULI ZA SERIKALI NA BINAFSI**

MWAKA	SKULI ZA SERIKALI			SKULI ZA BINAFSI			JUMLA		
	IDADI YA WANAFUNZI	IDADI YA WALIMU	WFUNZI KWA WALIMU	IDADI YA WANAFUNZI	IDADI YA WALIMU	WFUNZI KWA WALIMU	IDADI YA WANAFUNZI	IDADI YA WALIMU	WFUNZI KWA WALIMU
2017	341,870	10,274	33	35,970	2,266	16	377,840	12,540	30
2018	361,631	10,733	34	42,251	2,427	17	403,882	13,160	31
2019	379,845	11472	33	46,038	2958	16	425,883	14,430	30
2020	392,066	12128	32	51,203	3542	14	443,269	15670	28
2021	407,329	12828	32	53,473	3321	16	460,802	16149	29

JADWELI NAM. 6a(i)

MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 2, 2016- 2020

MWAKA	WATAHINIWA			WALIOFAULU			KIMA CHA KUFAULU (%)		
	WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA	WAV	WAS	JUMLA
2016	11673	13414	25087	7497	10084	17581	64.2	75.2	70.1
2017	20514	26056	46570	13670	20791	34461	66.6	79.8	74.0
2018	15211	17425	32636	9921	13986	23907	65.2	80.3	73.3
2019	14725	17751	32476	10017	14929	24946	68.0	84.1	76.8
2020	17736	14543	32279	15107	10286	25393	85.2	70.7	78.7

JADWELI NAM. 6a(ii)**NAFASI ZA SKULI KUMI BORA KATIKA MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA PILI (2016 - 2020)**

NAFASI	2016	2017		2018	2019	2020
		STD VI	STD VII			
1	Fidel Castro	Fidel Castro	Fidel Castro	Lumumba	Lumumba	Fidel Castro
2	Lumumba	Lumumba	Lumumba	Fidel Castro	Fidel Castro	Lumumba
3	Madungu "B"	Tumejuja	S.O.S Hermann	Moh'd Juma Pindua	Mikindani Dole	Moh'd Juma Pindua
4	Zanzibar Ccommercial	Tumejuja	Chasasa 'B'	Feza	Feza	Madungu
5	Mikunguni	Ben-bella	Laureat International	Mikindani Dole	Madungu	Mikindani Dole
6	Ben-bella	Mikunguni	Mahad Istiqama	Zanzibar Commcial	Moh'd Juma Pindua	Zanzibar Commcial
7	Chasasa	Kiembesamaki Islamic	Ben-bella	Chasasa 'B'	Bishara	Tumejuja
8	Tumejuja	Mahad Istiqama	Sunny Madressa	Ben-bella	Tumejuja	GLORIUS ACADEMY
9	S.O.S Hermann	Zanzibar Commercial	Francis Maria	Brilliant Academy	Chasasa 'B'	Kiembesamaki Islamic
10	High-view International	Chasasa 'B'	J.K.U	Mikunguni	S.O.S Hermann	Ben-bella

JADWELI NAM. 6(b)(i)**MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 4, 2016 - 2020 WAVULANA**

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU (%)				
		DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA DIV.I-IV	DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA DIV. I-IV
2016	6207	145	450	891	2954	4440	2.3	7.2	14.4	47.6	71.5
2017	6905	85	433	849	3429	4796	1.2	6.3	12.3	49.7	69.5
2018	7444	112	463	1054	3478	5107	1.5	6.2	14.2	46.7	68.6
2019	10433	154	711	1307	5236	7408	1.5	6.8	12.5	50.2	71.0
2020	9587	117	399	874	4100	5490	1.2	4.2	9.1	42.8	57.3

JADWELI NAM. 6(b)(ii)**MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 4, 2016 - 2020. WASICHANA**

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU (%)				
		DIV.I	DIV.II	DIV.III	DIV.IV	JUMLA	DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA
2016	7835	97	411	995	4150	5653	1.24	5.25	12.70	52.97	72.2
2017	9541	70	370	907	4930	6277	0.73	3.88	9.51	51.67	65.8
2018	9824	73	422	1151	5273	6919	0.74	4.30	11.72	53.67	70.4
2019	17461	145	801	1596	8651	11193	0.83	4.59	9.14	49.54	64.1
2020	13982	113	517	1011	6117	7758	0.81	3.70	7.23	43.75	55.5

JADWELI NAM. 6(b)(iii)

MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 4, 2016 - 2020
JUMLA YA WAVULANA NA WASICHANA

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU (%)				
		DIV.I	DIV.II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA	DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA
						DIV. I - IV					DIV. I - IV
2016	14042	242	861	1886	7104	10093	1.72	6.13	13.43	50.59	71.9
2017	16446	155	803	1756	8359	11073	1.47	4.88	10.68	50.83	67.3
2018	17268	185	885	2205	8751	12026	1.40	5.13	12.77	50.68	69.6
2019	27894	299	1512	2903	13887	18601	0.87	5.42	10.41	49.78	66.7
2020	23569	230	916	1885	10217	13248	0.98	3.89	8.00	43.35	56.2

JADWELI NAM. 6(c)(i)

MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 6, 2016/17 - 2020/2021 WAVULANA

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU U(%)				
		DIV.I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA DIV. I - IV	DIV.I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA DIV. I - IV
2016/17	985	33	213	515	130	891	3.4	21.6	52.3	13.2	90.5
2017/18	777	43	188	370	79	680	5.5	24.2	47.6	10.2	87.5
2018/19	871	77	256	476	41	850	8.8	29.4	54.6	4.7	97.6
2019/20	1030	98	310	509	71	988	9.5	30.1	49.4	6.9	95.9
2020/21	1312	70	370	664	121	1225	5.3	28.2	50.6	9.2	93.4

JADWELI NAM. 6(c)(ii)

MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 6, 2016/17 - 2020/21 WASICHANA

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU (%)				
		DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA	DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA
DIV. I - IV	DIV. I - IV	DIV. I - IV	DIV. I - IV								
2016/17	978	17	164	612	128	921	1.7	16.8	62.6	13.1	94.2
2017/18	727	45	167	425	78	715	6.2	23.0	58.5	10.7	98.3
2018/19	938	48	251	576	51	926	5.1	26.8	61.4	5.4	98.7
2019/20	1060	90	303	527	92	1012	8.5	28.6	49.7	8.7	95.5
2020/21	1358	54	405	764	90	1313	4.0	29.8	56.3	6.6	96.7

JADWELI NAM. 6(c)(iii)**MATOKEO YA MTIHANI WA KIDATO CHA 6, 2016/17 - 2020/21 JUMLA YA WAVULANA NA WASICHANA**

MWAKA	WATAHINIWA	WALIOFAULU					KIMA CHA KUFAULU (%)				
		DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA	DIV.I	DIV. II	DIV. III	DIV. IV	JUMLA
		DIV. I	DIV. II	DIV. III	DIV.IV	DIV. I - IV				DIV. I - IV	
2016/17	1963	50	377	1127	258	1812	2.5	19.2	57.4	13.1	92.3
2017/18	1504	88	355	795	157	1395	5.9	23.6	52.9	10.4	92.8
2018/19	1809	125	507	1052	92	1776	6.9	28.0	58.2	5.1	98.2
2019/20	2090	188	613	1036	163	2000	9.0	29.3	49.6	7.8	95.7
2020/21	2670	124	775	1428	211	2538	4.6	29.0	53.5	7.9	95.1

JADWELI NAM. 6(d)**MATOKEO YA MITIHANI MINGINE YA TAIFA YA TANZANIA 2016/17 - 2020/21**

MWAKA	FTC / DIPLOMA YA UFUNDI NTA 6				UALIMU DIPLOMA			
	WATAHINIWA		WALIOFAULU		WATAHINIWA		WALIOFAULU	
	WAS	JUMLA	WAS	JUMLA	WAS	JUMLA	WAS	JUMLA
2016/17	32	110	27	91	313	390	254	321
			(84.4%)	(82.7%)			(81.1%)	(82.3%)
2017/18	38	104	32	80	203	245	144	175
			(84.2%)	(76.9%)			(70.9%)	(71.4%)
2018/19	39	128	38	118	142	176	102	129
			(97.4%)	(92.2%)			(71.8%)	(73.3%)
2019/20	30	107	30	105	206	323	191	302
			(100.0%)	(98.1%)			(92.7%)	(93.5%)
2020/21	104	548	73	388	241	314	233	305
			(70.2%)	(70.8%)			(96.7%)	(97.1%)

JADWELI NAM. 7

MATOKEO YA MTIHANI KWA WATAHINIWA WA FARAGHA KIDATO CHA 4 VITUO VYA ZANZIBAR, 2016- 2020

WILAYA	2016			2017			2018			2019			2020		
	WFANYA	WFAULU	%												
MJINI	1017	392	38.5	1111	618	55.6	1339	552	41.2	1294	467	36.1	1082	628	58.0
MAGHARIBI'A'	1071	559	52.2	1198	736	61.4	1291	698	54.1	437	213	48.7	466	317	68.0
MAGHARIBI'B'	-	-	-	-	-	-	-	-	-	802	322	40.1	872	540	61.9
KASKAZINI'A'	210	74	35.2	199	110	55.3	202	72	35.6	152	50	32.9	93	45	48.4
